JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE

Kumb.Na.KTV/MLDC/S.10/29/32 23/07/2025

## TANGAZO LA NAFASI YA AJIRA YA MKATABA WA MUDA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele anakaribisha maombi ya nafasi za kazi za ajira ya mkataba kwa wananchi wote wa Mkoa wa Katavi wenye sifa za kujaza nafasi hizo. Nafasi zinazotangazwa ni kama zilizoorodheshwa hapa chini:-

### 1.0. MKUSANYA USHURU (NAFASI 12)

#### 1.1.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kukusanya ushuru na mapato katika eneo atakalopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji.

ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu.

iii. Kutunza vizuri mashine za kukusanyia mapato (POS).

iv. Kuwasilisha makusanyo katika akaunti za Halmashauri (ku-benki fedha za makusanyo kila siku)

v. Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Mkurugenzi Mtendaji.

vi. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na msimamizi wa kazi.

#### 1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) na kupata cheti cha kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI). Awe na taaluma ya Uhasibu au Biashara kuanzia ngazi ya cheti na kuendelea, mwenye uadilifu na asiye na kasoro yoyote. Mwombaji mwenye mafunzo ya Jeshi la Akiba atapewa kipaumbele.

#### 1.1.3 UJIRA

Kama itakavyoamuliwa katika majadiliano baina ya mwajiri na mwajiriwa.

Scanned with CamScanner

## 2. DEREVA II (NAFASI 05)

### 2.2.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.

ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.

iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.

iv. Kufanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika.

v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.

vi. Kufanya usafi wa gari na

vii. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri.

### 2.2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 2.2.3 UJIRA

Kama itakavyoamuliwa katika majadiliano baina ya mwajiri na mwajiriwa.

### MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wakazi wa Mkoa wa Katavi na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.

iii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi (CV) awe na anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana pamoja na barua za wadhamini watatu wa kuaminika zikiwa na nakala za kadi ya kitambulisho cha mpiga kura.

iv. Mwombaji awe tayari kupangwa na kubadilishiwa kituo kadri ya mahitaji ya mwajiri.

v. Mwombaji aambatishe kivuli cha kitambulisho cha NIDA au Kitambulisho cha Mpiga Kura na picha mbili za rangi (Passport size)

Scanned with CamScanner

vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya vya Elimu na Taaluma ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne au sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya taaluma kwa kada husika.

vii. "Testmonial","Provisional Results", Statement of results", hati ya matokeo ya kidato cha nne au kidato cha sita havitakubalika.

viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **04 Agosti,2025 saa 9:00 Alasiri.**

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi zinatakiwa kuwa na anuani kamili ya mwombaji,namba za simu, na zipitishwe au kupitia kwa Mtendaji wa Kata/Kijiji unachoishi. Pia maombi yote yawasilishwe kwa **mkono** katika Ofisi ya **Mkurugenzi Mtendaji (MASIJALA).**

Sigilinda M. Mdemu
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) MLELE

Scanned with CamScanner